



**REPUBLIC OF KENYA**  
**COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI**  
**SECOND ASSEMBLY –THIRD SESSION**

**THE HANSARD**

**Tuesday, 27<sup>th</sup> August 2019**

*The House met at the County Assembly Chamber,  
Malindi Town, at 2:30 p.m.*

*[The Temporary Speaker (Hon. Mumba) in the Chair]*

**PRAYERS**

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Good afternoon hon. Members. Welcome to the afternoon sitting.

**MOTION**

**ADOPTION OF THE REPORT ON THE STATUS  
OF FIRE STATIONS IN KILIFI COUNTY**

**Hon. Mwamtsi:** Mr. Speaker, I want to present to the House a Motion in regards to the adoption of the Report of the Sectoral Committee on Roads, Transport and Public Works on the status of fire stations in Kilifi County. I pray that this House adopts the Report of the Sectoral Committee on Roads, Transport and Public Works on the status of fire stations in Kilifi County laid down on the Table of this House on the 19<sup>th</sup> of August, 2019.

In regards to that, I seek hon. *Sonko* Member for Marafa to second.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Hon. Member, based on the composition of the Members in this House and those present there is no member called *Sonko*.

**Hon. Mwamtsi:** The member is hon. Renson Kambi (Karisa) but *Sonko* is his alias name.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Okay thank you.

*(Hon. Karisa seconded)*

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

*(Question proposed)*

**Hon. Mwamtsi:** Mr. Speaker, the Committee on Roads, Transport and Public Works drives its mandate from Standing Order No. 194 (5). Again, the Fourth Schedule of the Constitution delegated fire and rescue operations to the county governments under the Department of Roads, Housing and Public Works. To just give a brief overview; this Department of Fire and Rescue Operations within the County Government of Kilifi has 73 members of staff. And within the County of Kilifi we have four fire stations, namely; Malindi, Kilifi, Mariakani and Mtwapa.

The Committee went on a research moving across all the fire stations around Kilifi County and came up with some findings that resulted to this Motion. The Committee identified a number of problems. One; there were no adequate fire fighting engines. Two; out of the 73 members of staff, very few had undergone training in regards to fighting fires and rescue operations. Again, it is required that wherever there is a fire station there is a source of water called a hydrant.

We saw that there were very few hydrants and if there were there, they were not close to the fire station. Fire fighting is a very dangerous exercise. It is required that whenever there is a fire station, there are also ambulances accompanying the fire engines. We found that there was no single fire station that had an ambulance in case of an emergency. Fire fighting men and women are supposed to be next to the fire station and they require accommodation. The Committee found that in these fire stations, there were inadequate accommodation facilities to house the members of staff that are supposed to fight in case of fire.

The Committee also found that there was no direct communication line that in case of an emergency, a member of the public in distress could make a call. Like in the case of a fire station within Kilifi North, a phone number had been indicated on the van of which when you call, it was answered by someone who was not even in Kilifi County. We have had a number of fires within Kilifi County, the recent one was at Mtwapa, Malindi and Kilifi; even for a member of this House, his house was burnt down by fire and our fire fighting facilities could not rescue it because of the challenges that this Department was facing.

We had some sittings together with the stakeholders in this area and we came up with some recommendations that; one this House agrees with our Report and that the CEC Member in charge of Roads, Transport and Public Works develops a Policy that will make all public institutions within Kilifi County have hydrants. Secondly, all schools have boreholes so that they could be used as hydrants incase of fire.

Thirdly, the County Government must ensure that in every fire station there is a hydrant that supplies water to that fire station. The Committee recommends that the Department of Roads, Transport and Public Works prioritizes within its budget the purchase of new fire fighting engines because the existing ones are ineffective or faulty. The Committee recommends that the Department of Roads, Transport and Public Works comes up with a toll free line like the 999 used by the central government where when you press that number it will go to the command centre ready to respond to cases of fire. I wish to stop there and allow other Members to contribute.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Yes hon. Karisa.

**Hon. Karisa:** Asante Mhehsimiwa Spika. Nasimama kuwaambia wenzangu tuunge mkono Ripoti hii ambayo ni ya manufaa kwetu. Mheshimiwa *pastor* ni mmoja wapo ambaye

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

mkasa ulimpata na hatukuweza kupeleka wazima moto kwa wakati ufaao. Tumeona ya kwamba kuna umuhimu wa kuunga Ripoti hii mkono hata mwaka wa kifedha unaokuja...

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Yes hon. (Ms.) Messo what is it?

**Hon. (Ms.) Messo:** Thank you so much Mr. Speaker. I just want to correct the Member on the Floor that hon. Benson is not a pastor; he is a Bishop, so do not lower his dignity please.

**Hon. Karisa:** Asante sana kwa kunijua. Nilikuwa namwita *pastor* kwa sababu sikuwa najua. Labda mlikuwa pamoja mkaelezana kuwa yeye sio *pastor* ni Bishop. Kwa sasa nimepata ufahamu kwamba hon. Benson ni *Bishop* shukruni.

Kama nilivyoelezea kwamba hon. *Bishop* alipata mkasa na kwa sababu ya mambo ambayo yamenukuliwa hapa, tuliona ni vyema kila kituo cha wazima moto kuwe na visima. Mbali na hivyo kuwe na mabirika ya maji yasiyopungua lita elfu mia tano (500,000) kwa sababu ya zile changamoto tunazozipata. Kuna wakati moto hutokezea magari hayana maji. Itakuwa vyema tupate mabirika ya maji ili kusaidia. Tafadhali waheshimiwa tuunge mkono Ripoti hii na tupitische kwa manufaa ya watu wa Kilifi.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Hon. Ms. Victoria.

**Hon. (Ms.) Victoria:** Thank you Mr. Speaker for giving me this opportunity to contribute to the Motion. I am supporting this Motion because the current situation in the fire stations in this county is pathetic. The working conditions at the fire stations are not conducive for the staff. Listening to their stories you can even weep. They depend on the same water being used to put out fire. This happens especially in Mariakani fire station when there is no water to put out fire they also do not have drinking water.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Hon. Member, are you trying to say that this is the reason as to why the engines lack water whenever fire breaks because they use the same water that is supposed to put the fire out?

**Hon. (Ms.) Victoria:** Yes, we are dealing with the whole fire Department. We cannot have a fire station without workers. If the workers are complaining, how do you expect good performance? They even said they lack the safety equipment supposed to be used in a fire outbreak. Most go without any safety garments and boots. In case one has got an accident during that exercise, they have to leave the exercise and attend to the patient. This means if people are in, the house will continue burning.

I urge the Department to equip the fire stations with ambulances so in case of an accident the patient is carried and the exercise is in a position to go on. Even the fire engines had problems. Some were leaking and some were grounded when we asked we were told that there was no money to maintain them. If you make a follow up, there are just minor issues affecting the engines. We are experiencing loss in our county because this Department has not been well equipped.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Are you talking about the Department because we are only concentrating on the fire stations. When you say the Department it means the Department of Roads, Transport and Public Works and as far as I know there are lots of funds allocated to that Department. When you are talking, strictly concentrate on the section of fire station. Is it the one that is not given enough funds for it now to be equipped or the Department?

**Hon. (Ms.) Victoria:** Yes I am basing on the area of the fire stations.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): What is your point of Order hon. Member for Garashi?

**Hon. ziro:** Thank you Mr. Speaker. Maybe instead of confusing her more you could even allow her to speak in Swahili because in her explanations she does not come out clearly. I

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

personally do not understand what she is trying to tell this House. I am not trying to embarrass her.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Yes, you have made your point but I think she is in a position to tell us which language she is more comfortable to use.

**Hon. (Ms.) Victoria:** Thank you Mr. Speaker, Sir. I do not know Kiswahili. I wish I was more conversant in Kiswahili. He will have to see me after this session so that I can explain to him what I mean.

So I was talking on the status of our fires stations; it is not pleasing right from the staff to the machinery. So I urge the Members to support this Motion because it affects almost all of us. Thank you Mr. Speaker, Sir for allowing me to use English because you know my problem very well.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Thank you. Yes hon. Mary Maneno.

**Hon. (Ms.) Maneno:** Asante sana Bw. Spika kwa nafasi hii. Mimi ni Mwanakamati wa Barabara na hakika Mwenyekiti na Kamati yake walifanya kazi nzuri nikiwa mmoja wao. Tulizunguka Mtwapa, Kilifi, Mariakani na hata Malindi lakini hakika hali ambayo tuliiona haikuwa ya kuridhisha...

*(Hon. (Ms.) Ngari stood on a Point of Order)*

**Hon. (Ms.) Ngari:** Asante. Labda mheshimiwa anayezungumza anatuambia kwamba walizunguka Kilifi, Mombasa na sijui walikuwa wanazunguka nini? Labda atuelezee...

**Hon. (Ms.) Maneno:** Bw. Spika naomba nimjibu. Nafikiri akili yake haikuwa hapa...

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Subiri kwanza mheshimiwa. Mheshimiwa Loice (Ms. Ngari) naomba unisikilize; unapopewa nafasi ya kuzungumza kwa Hoja ya nidhamu tafadhali naomba pia uwe makini wakati mheshimiwa mwenzako anazungumza ili uweze kunukuu haswa ni kipi kilichotoka katika mazungumzo yake kinyume na Kanuni za hili Bunge. Kadri nilivyomsikia alikuwa bado anajieleza na haja taja Mombasa. Kwa hivyo, nafikiri wewe ndio umepotoka na ningepomba umruhusu aendelee kuzungumza kisha baadaye utaweza kumfahamu vyema. Endelea mheshimiwa.

**Hon. (Ms.) Maneno:** Asante sana Bw. Spika kwa kunikinga kutoka mheshimiwa Loice (Ms. Ngari) maana hakuwa hapa kwa uhakika. Tumetembelea hivyo vituo vya moto na havikuwa vya kuridhisha. Ukiangalia hata zile nambari za simu zilizokuwa kwa yale magari ya kuzima moto, hazikuwa zinafanya haswa kituo cha Mariakani.

Kwa hivyo, msimamizi wa kile kituo inalazimu atumie simu yake ya mkononi akifanya kazi masaa yake yakiisha akienda nyumbani kama simu yake haina moto basi inabidi aizime na aipeleke kwa moto. Kunapotokea janga lolote la moto, Kaunti ya Kilifi ama Mariakani basi hapatikani na wananchi wanazidi kuumia.

Katika Kamati ukiangalia mapendekezo nambari saba ukurasa wa 11 ni lazima kuwe na mnara au simu maalumu ambayo mwananchi anaweza kuwafikia katika zile afisi zao na akapata usaidizi wa haraka. Na tuhakikishe kwamba hizi afisi zao ziwe na sehemu ambayo kutakuwa na ule utekelezaji wa yale mahusiano ili mwananchi apate huduma.

Mengi yamesemwa na walionitangulia. Ombi langu kwa Bunge hili ni tuunge mkono hii ili ipite. Na vile vile naomba Kamati ya utekelezaji (*Implementation*), wachukulie haya mapendekezo kwa uzito ili wananchi wa Kilifi wapate kusaidika zaidi. Tumepewa mfano hapa wa mheshimiwa Benson (Chengo) ambaye alipata mkasa na hakuna alichookoa kwa sababu ya shida kama hizi ambazo waheshimiwa wamezitaja, ikiwemo uhaba wa maji na ambulensi zile

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

zinazotakikana kuwa nyuma ya magari ya kuzima moto. Ningeomba Kamati hiyo ichukulie mambo haya kwa uzito na kuyafuatilia kwa ukaribu. Asante na ninaomba Bunge hili liunge mkono.

**Hon. Mramba:** Mheshimiwa Spika, mimi naunga maono Ripoti iliyoletwa na Mwenyekiti mheshimiwa John Mwamtsi ambaye anatoka kwa jamii ya walio wachache ama *minority* kwa lugha ya Kiingereza. Utendaji kazi wa kitengo kile cha wazima moto mara nyingi kimetuweka kama Kaunti vibaya sana maana tunaabika. Nyumba ikianza kuteketea na gari likifika pale halina maji, ama gari linaharibikia njiani ni hali isiyopendeza. Hivi majuzi kuliteketea nyumba nyingi sana za wazungu pale Casaurina. Gari lilipofika pale, nyumba zilikuwa zimeshachomeka kwa sababu lilikuwa limeenda kutafuta maji kwanza, mara hakuna *battery* na kadhalika. Yaani matatizo ni mengi.

Juzi moto ulishika Arabuko Sokoke hapa karibu na Jilore; gari lilipoenda likakwama kwenye mlima wa Kakuyuni, huku watu wakisubiri gari liende likazime moto. Kwa hivyo, inakuwa ni aibu kila mara. Ninavyokumbuka mimi kabla ya Bunge la kwanza kuvunjwa kulinunuliwa *engine* sita mpya na zikaja zikawa *launched* pale uwanja wa Karisa Maitha.

Sijui zile *fire engines* zilizonunuliwa kama zilikuwa ziko namna gani maana ni juzi sana; haijazidi miaka mitatu kwani nakumbuka vizuri sana. Sasa tutakuwa tukitafuta pesa kununua *engines* labda ambazo hazistahili ama ni kitu gani? Tunastahili kuboresha ufanyajikazi wa kitengo hiki cha wazima moto. Kwanza, tuangalie masilahi ya wafanyikazi na tuone haya magari ya kuzima moto yafanyiwa ukaguzi mara kwa mara ili kwenye matatizo yajulikane mapema. Tatizo hili limeharibu utalii hapa Malindi.

Bwana Spika, nikikwambia hivi ni kwamba, wakati ule mtu alikuwa akikata leseni ya biashara ni lazima alipe pesa ya wazima moto. Kuna cheti cha moto kilikuwa lazima mtu akilipie ndiyo mtu apewe leseni. Moto ulikuwa ukishika mahali hakuna gari ya kaunti ya kuzima moto itakuja.

Bwana Spika, hiyo si haki. Tunachukua pesa za mwananchi na hatuwezi wapa hiyo huduma ambayo wana haki ya kuipata. Naomba tupitishie hii Ripoti na tuboresha kitengo hiki cha wazima moto ili kiweze kutusaidia. Watalii sasa hivi wamepeana sababu mojawapo kuwa Malindi haiko salama kuishi. Moto ukishika nyumba, gari ya wazima moto labda itakuja baada ya saa mbili na nyumba itakuwa ishakwisha waka moto yote. Naomba tuweze kupitisha Hoja hii ili tuweze kuboresha hiki kitengo cha wazima moto. Asante.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Mheshimiwa Margret wakati ni wako.

**Hon. (Ms.) Margaret:** Asante Mheshimiwa Spika kwa hii nafasi. Umenichelewesha maana nilikuwa nataka kumjuza Mheshimiwa wa Kakuyuni. Mheshimiwa wa Kakuyuni amevaa kislamu lakini sasa kofia ameiweka chini. Sasa saa hii hiyo kanzu imetoka ni kama amevaa dera. Asante.

*(Laughter)*

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Sasa mheshimiwa Margret (Dama) mimi nilidhani umesimama ili kutoa changizo katika Mswada ambao tunaujadili. Unajua inakuwa vigumu kuweza kujua kama ni Hoja ya Nidhamu ama ni vipi wakati mkono umeunyosha maana hapo sikujua wataka kuzungumza ama ni Hoja ya Nidhamu. Ungekuwa umezungumza. Kwa kuwa ashakaa tayari kwa hivyo hiyo Hoja yako ya Nidhamu haina nafasi kwa sasa. Asante. Mheshimiwa Benson (Chengo) endelea.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

**Hon. Chengo:** Asante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia hii nafasi angalau nami nichangie Hoja hii. Mimi nimesimama kuunga mkono hii Ripoti. Mimi ni mmoja wa wale ambao walipata mkasa wa moto. Shida kubwa ilikuwa ni mawasiliano. Moto ulianza kwa chumba cha mpangaji wangu mhandisi Joseph Waziri.

Mhandisi Joseph Waziri hakuwa na namba ya wazima moto. Alipigia katibu wa kitengo hicho na ilichukua mda hawa watu wa kuzima moto kupatikana. Mawasiliano ama namba ya simu ya wazima moto ni muhimu ili wakati moto ukitokea mawasiliano yafanyike ndo moto uzimwe haraka.

Lengine ni juu ya maji. Walipokuja ile safari ya kwanza walijaribu kuzima na maji yakaisha. Kulikuwa na vurugu kwa sababu wananchi walikasirika kwa sababu gari limekuja na halina maji; walitaka kupigwa wakati huo wakatoroka.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Mheshimiwa pengine kwa kuweka wazi tu, unasema maji yalikwisha ama gari lilikuwa halina maji?

**Hon. Chengo:** Walikuja na maji lakini yakaisha na nyumba ikawa yaendelea kuchomeka walikuwa hawajaizima.

**The Temporary Speaker** (Mumba): Shukrani, unaweza endelea.

**Hon. Chengo:** Sasa walipokuwa wanatoka kukawa na vurugu maana wananchi walighadhabika kwa sababu nyumba ilikuwa yachomeka na hao walikuwa wamekuja na maji kidogo.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Mheshimiwa ungeruhusu upewe habari zaidi?

**Hon. Chengo:** Hapana hii habari ambayo ninayo yanitoshia.

*(Laughter)*

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Unaeza endelea mheshimiwa.

**Hon. Chengo:** Kwa hivyo, ninachosema ni kila sehemu iwe na maji ili panapotokea moto uwe waweza zimwa haraka. Shida ni kuwa panapotokea moto, maji mpaka yakatafutwe na wanaporudi huwa nyumba imechomeka. Lengine pia ni kuhusu wafanyikazi; kwa kweli ni kidogo wanastahili kuongezwa.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Mheshimiwa wa Garashi wakati ni wako. Mheshimiwa Chengo naomba ukae.

**Hon. Ziro:** Asante Mheshimiwa Spika. Kabla sijatoa Hoja yangu naomba kumpa pole Mheshimiwa askofu Benson Chengo ambaye aliweza kupata huu mkasa. Naomba kumuuliza yeye akiwa askofu, ni kweli kama mtu hatoi fungu la kumi Mungu anaweza kumuadhibu kwa njia hiyo? Yeye ni askofu na anaweza kutueleza jambo hilo. Asante.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Naomba umrudishie kipaza sauti mheshimiwa Benson (Chengo); naomba uendelee kutoa changizo zako na maswala ya dini tutayapatia nafasi wakati wake.

**Hon. Chengo:** Asante sana Mheshimiwa Spika. Akiwa na maswali hayo anitafute wakati mwengine nitamjibu. Tulikuwa tumesema wafanyikazi ni kidogo; angalau wangukuwa kwa *shift* tatu wanaweza kusaidia zaidi. Wengine hukusha tena wakashinda kazini sasa kunapotokea jambo la ghafla wengi huwa wachovu sana. Walikuwa wanaomba wawe kwa *shift* tatu ili ziwaisaidie wakati kama kumetoa janga la moto wawe wanaweza fanya haraka maana watakuwa si wachovu.

Ulinzi ni muhimu pia kwao wawe wakienda kuzima moto waandamane na askari maana wakati wakienda kuzima moto na wakiwa hawana vifaa maalumu vya kuzima moto, basi

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

wananchi huwa na ari ya kuwapiga. Nasimama kuunga mkono Hoja hii. Asante na Mungu awabariki.

**The Temporary Speaker** (Hon.Mumba): Shukrani. Mheshimiwa Mwambire wakati ni wako.

**Hon. Mwambire:** Asante Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii. Nasimama kuunga mkono na kupongeza Kamati ambayo imekuja na mapendekezo ya kuboresha maswala ya kuzima moto. Janga la moto hapa Kilifi limekuwa likitokezea na ni katika matukio machache sana moto umeweza kukabidhiwa. Nimepitia haya mapendekezo ya Kamati na nimeona kwamba mapendekezo haya yakiwa yataweza kutekelezeka basi huenda yakapunguza vile visa vya moto. Nikimaanisha kwamba yale matokeo ya kukabili moto yanaweza boreka zaidi. Jambo moja ambalo nimelipitia hapa lakini sikuweza kuliona ni kwamba katika zile sehemu ambazo zimeendelea huwa kunawekwa *signal* katika kila nyumba za biashara ambazo *signal* zile huwa zinapeleka ujumbe moja kwa moja mpaka *fire stations*.

Kwa hivyo, mimi naunga mkono haya mambo ya *24 hour emergency hotline*. Huenda ikaweza kukabili hali hiyo. Kuna haja kwamba hawa wasimamizi wa kuzima moto waweze kuwekewa sheria kwamba wakati wowote wanakuwa na umakini wa kuona kwamba wako na vile vifaa ambavyo vinahitajika waweze kuwa navyo. Kwa hivyo, nasimama kuunga mkono jarida hili likaweze kupitishwa katika Bunge hili. Idara hii iweze kutekeleza kikamilifu. Asante Bw. Spika.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Mheshimiwa, unaunga mkono jarida ama Mswada? Nafikiri ni Mswada ndio ulioko mbele sasa hivi kwa hivyo asante kwa changizo zako.

**Hon. Mwambire:** Naunga mkono Mswada huu ambao uko katika jarida hili tuweze kuupitisha.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Hon. Alphonse Mwayaa.

**Hon. Mwayaa:** Asante mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi hii ili kwamba nami niweze kuunga mkono Mswada ambao umeletwa na Kamati yetu ya Barabara. Mheshimiwa Spika, kwa kweli Kilifi Kaunti tumepoteza raslimali nyingi sana kupitia mambo ya moto na tumeona kwamba katika kitengo hiki ambacho ni cha wazima moto mara nyingi hakijatusaidia. Ni juzi tu kule maeneo yangu kuna nyumba ya mwana biashara mmoja ambayo iliungua na kulikuwa na mali nyingi maanake ilikuwa ni duka hapo na kusema la kweli tulijaribu kupiga simu kama wenzangu walivyosema Mariakani na simu ilikuwa ni kama ambaye haifanyi kazi.

Kwa hivyo, hiki kitengo cha wazima moto hakijatusaidia vile; ndio maana nikasema naunga mkono ikiwa vile vifaa ambavyo wamesema Kamati vikinunuliwa vinaweza kusaidia basi vinunuliwe ili viweze kusaidia. Maji yaweze kuchimbwa tuweze kupata maji ya kutosha vifaa viweze kununuliwa ili kwamba tuweze kusonga mbele kama watu wa Kilifi. La kuongezea mheshimiwa Spika, kuna muimbaji mmoja aliyeimba akasema kwamba nyama ya bata ni tamu. Huyu muimbaji siku moja aliimba pale *show* kukawa kunamwanasiasa mashuhuri sana akaenda kumtuza yule mtu kisha akamwambia hii nyimbo ya nyama ya bata ni tamu tumeisikia ukirudi katunge nyimbo ya kuku nayo tusikie naye kuku yuko namna gani.

Nataka niwatume Kamati yetu ya Usafiri; tuko na matingatanga yetu ambayo pia yanahusu mambo ya barabara wakirudi waende wakaandike hizi tingatinga zinafanya kazi namna gani hapa Kilifi maanake kwengine barabara zetu hazipitiki. Kwa hivyo, leo tunaimbiwa nyama ya bata ni tamu sawa tumejua kwamba ni tamu na tutaunga mkono Ripoti hii lakini mkirudi Kamati ya Usafiri kaimbeni nyimbo nyingine ya hizi tingatinga zetu zitalima vipi barabara za Kilifi kwani kwengine hakupitiki? Ni nyinyi Kamati ambayo inashughulika na mambo haya. Haya ya leo tunayaunga mkono mambo ya kitengo cha wazima moto. Na mkirudi

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

kapange taratibu kamili ya hizi tingatinga zetu na hata tuliunga mkono ndani ya Bunge hili ili kwamba yaweze kufanyia kazi watu wa Kilifi. Kwa hivyo, katungeni nyimbo mpya tena lakini hii tunawaunga mkono na tunaimba pamoja. Mungu awabariki kwa kazi nzuri. Asante naunga mkono.

*(Question put and agreed into)*

## **COMMUNICATION FROM THE CHAIR**

### **FRIENDLY MATCHES**

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Hon. Members, I wish to make the following Communication; today being Tuesday, I am informed that all roads are leading to the field; there are friendly matches there for all disciplines as we prepare for CASA (County Assembly Sports Association) games. So we are requested that we all attend as we prepare for the games.

## **ADJOURNMENT**

Thank you and in the absence of any other business in the Order Paper, this House stands adjourned until tomorrow 28<sup>th</sup> August at 2:30 p.m. Thank you and have a good evening.

**The House rose at 3:35 p.m.**